# Usawiri wa Wanaume katika Methali za Kijinsia za Jamii ya Wanyankole: Mtazamo wa Ubabe- Dume

*Arinaitwe Annensia, Mosol Kandagor na Magdaline Wafula*
*Chuo Kikuu cha Moi*

**Ikisiri**

**Makala haya yamechunguza namna wanaume wanavyosawiriwa katika methali za kijinsia, zinavyoweza kujitokeza katika miktadha tofauti ndani ya jamii ya Wanyankole. Mkabala wa kinadharia uliotumika katika uhakiki na uchanganuzi wa data ni nadharia ya Uwezo-Uume. Makala haya yalichunguza na kuhakiki methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole zilizoegemea jinsia ya kiume. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kwamba, jamii ya Wanyankole imekuwa ikitumia methali za kijinsia katika shughuli zake tofauti. Makala haya yamepambanua miktadha za jamii ya Wanyankole zinazoathiri usawiri wa wanaume. Miktadha hizi ni kama ni pamoja na ndoa, utamaduni, malezi na maadili, elimu, uchumi, na uongozi. Mwisho makala haya imebainisha namna na sababu ambavyo methali hizi za kijinsia zilivyowasawiri wanaume katika jamii ya Wanyankole.**

**Maneno Muhimu:** Usawiri, Methali, Kijinsia, Uwezo-Uume

## Utangulizi

Methali, ngano, visasili, mighani na vitendawili ni usanii wa msemaji au sanaa ya usemaji inayopatikana katika kipengele cha fasihi simulizi. Haya ni maoni ya Bascom (1955) katika Finnegan, (1992). Methali ni sehemu ya lugha na hutumika kuyatafakari, kuyapima maisha na kufunzia jumuiya. Abdilatif (1978) katika Wandera (1996) anadai kuwa hakuna fasihi iliyochipuka na kuendelea kuishi katika ombwe tupu. Fasihi yoyote ile hupata uhai wake katika jamii inayohusika. Jamii ya Wanyankole ni miongoni mwa jamii nyingi katika bara la Afrika, ambazo bado zinahifadhi kipera hiki cha fasihi simulizi na kukitumia kutekeleza majukumu mbalimbali kama vile kuelemisha, kuburudisha na kuonya wanajamii. Hata hivyo, sawa na jamii nyinginezo katika bara la afrika, methali za Wanyankole aghalabu hutungwa katika misingi ya kijinsia. Katika Jamii hii, inaaminika kuwa kuna aina mbili za jinsia: Jinsia ya Kiume na Jinsia ya Kike. Kwa hiyo ni kutokana na mkabala huo ndipo makala haya yalizuuumu kuchunguza usawiri wa wanaume katika methali za kijinsia za Wanyankole.

Sababu kuu ya kuchunguza methali hizi za kijinsia katika jamii hii ni kwamba, tangu jadi jamii ya Wanyankole imetambulika kuwa miongoni mwa jamii ambazo zimejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni, ambao unaendeleza kipengele cha Ubabe-dume katika kila jambo ndani ya jamii. Huku ni kusema kwamba, wanaume katika jamii ya Wanyankole walienziwa na kupewa hadhi ya juu huku wanawake wakidhalilishwa na kupewa hadhi ya chini katika kila jambo ndani ya jamii hii. Hata hivyo taifiti za awali (Seita 1987; Lubuuka, 2010) zilijikita tu katika usawiri wa mwanamke katika methali za kijinsia za wanayankole. Ni kwa msingi huu ndipo makala haya yamechunguza usawiri wa wanaume katika methali za kijinsia za Wanyankole ili kubaini iwapo mfumo wa jamii umejidhiri katika miundo ya methali hizi.

Jamii ya Wanyankole ni mojawapo ya jamii ambayo inazungumza lugha ya Runyankore na hupatikana nchini magharibi mwa Uganda. Jamii hii imekuwa ikitumia kipera cha fasihi simulizi ambacho ni methali katika kuelemisha, kuburudisha na kuonya wanajamii wake. Methali hizi zimekuwa zikitumika kijinsia katika nyanja mbalimbali ndani ya jamii kutokana na Ubabe-dume kama vile; kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni, kindoa na kidini. Nadharia ya uwezo-uume ulitumika katika kuhakiki data. Mwasisi wa nadharia hii ni Robert Bly (Wells & Holland, 2001). Nadharia hii iliiendelezwa na Izugbara mnamo mwaka wa 2005 *(Kibigo, Choge na Simiyu, 2019).* Nadharia hii inahusisha dhana mbili; Uwezo na Uume. Inarejelea uwezo ambao jamii mbalimbali

huwapa wanaume. Nadharia hii hubainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume, hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika (Kibigo, 2019). Hii ndiyo sababu ambayo huifanya jamii kumchukulia mwanamume kwa njia chanya na kumchukulia mwanamke kwa njia hasi. Izugbara (2005) katika Kibigo (2019) anadai kuwa kutokana na uume wake (dhakari), mwanamume husawiriwa kuwa na sifa kama vile, uwezo, uvumilivu, ushujaa na ujasiri huku mwanamke akichorwa kuwa na sifa kama za uoga, kutothubutu mambo na kadhalika Kwa hivyo itakadi na utamaduni katika jamii huegemea zaidi kumjenga mwanamme kuwa bora zaidi ya mwanamke.

**Mihimili ya Nadharia**

i. Itikadi za kijamii huongoza fikra kwamba, utawala wa mwanamume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulisho vya jinsia ya kiume maandishi, matukio na maelezo ya kihistoria kwa misingi ya jamii husika (Wells & Holland, 2001).

ii. Utamaduni, lugha, imani na desturi zimewawezesha wanaume kuwa watawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za rasilmali zenye thamani katika jamii kama vile, shamba, kazi, pesa na taasisi za kijamii zenye nguvu kama vile serikali na dini (Collins, 1971; Sokoloff, 1980).

iii. Majukumu yanapogawanywa kiuana, wanaume huweka utambulisho wao katika sura na mfano wa Mungu wa kiume kwa manufaa yao, wakisisitiza kwamba, 'Mungu wa kiume' alimpa mwanamume mwanamke kama mwenzi wake (Ruether, 1974).

iv. Sifa angama za uume na maeneo ya ubabedume yanayojitokeza katika desturi kwa jumla kupitia: maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi na kukidhia familia, kuwa na tajriba na shari ya kijinsia, ukakamavu, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani na kuthubutu mambo (Chafetz, 1974; Doyle, 1985).

Mihimili ya nadharia hii imejikita katika utamaduni, itikadi za jamii, mgawanyo wa mamlaka na uwezo wa kijinsia, mielekeo na matarajio ya jamii kumhusu kila mwanajamii ( Kibigo 2019, Choge na Simiyu, 2019). Makala haya yametumia mihimili minne inayojitokeza katika nadharia hii. Nadharia hii ilikuwa mwafaka kwa vile methali za Kijinsia za Wanyankole husheheni taasubi za kiume zinazotokana na hoja kuwa jamii ya Wanyankole kama ilivyo katika jamii nyingine za kiafrika imeegemea mno katika mfumo wa uumeni.

Msingi wa data katika utafiti huu ulikuwa ni methali zilizoteuliwa kimaksudi kutoka katika jamii ya Wanyankole. Utafiti huu ulihusisha methali za kijinsia zilizowahusu wanaume katika jamii ya Wanyankole. Uteuzi huo ulifanywa kimaksudi kwa sababu utafiti ulilenga kuchanganua methali zilizohusu jinsia ya kiume katika jamii ya wanyankole. Mbinu ya mahojiano ilitumiwa kukusanya data kutoka kwa watafitiwa kumi na wawili waliohojiwa katika utafiti huu. Mtafiti alianza kuainisha data iliyokusanywa kutoka katika makundi mawili makuu, yaani kati ya wahojiwa wa umri kati ya miaka (25-45) waliowasilisha jamii ya kisasa na vilevile wahojiwa wenye umri kati ya (50-80) waliowasilisha jamii ya kijadi ya Wanyankole.

**Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu uliibuka na matokeo kuhusu namna ambavyo wanaume wamesawiriwa katika jamii ya Wanyankole. Ilibainika kuwa methali husika zimewasawiri wanaume kwa njia anuwai kama ambavyo tumejadili katika sehemu ifuatayo.

**Maadili na Malezi**

Jamii ya Wanyankole kama mojawapo ya jamii nyingi za Kiafrika ilichukulia kipengele cha maadili na malezi kuwa ngao kuu katika kuendeleza familia na jamii kwa jumla. Kutokana na mgao wa kazi ndani ya jamii kijinsia, ilijitokeza kwamba mwanamke ndiye iliyekuwa nguzo kuu katika kuzaa na kulea watoto huku malezi yakiendana na maadili ya jamii pamoja na utamaduni wake tofauti na jinsia ya kiume. Maingi (2005) anadai kuwa mwanamme ndiye aliyeshirikishwa katika utoaji wa maamuzi muhimu katika jamii ya Wanyankole huku mwanamke akiwekwa pembeni. Hata hivyo, Maingi (Keshatajwa) anaendelea kudai kuwa mwanammke anasifiwa katika jamii hii kwa mchango wake wa kuwalea watoto nyumbani. Kutokana na mawazo haya, ni bayana kwamba mwanamke alipewa

jukumu muhimu la kuendeleza malezi na maadili katika jamii. Hata hivyo, makala hii inabaini kuwa zipo methali za kijinsia katika jamii ambazo zinadhirisha kuwa wanaume pia walichangia katika malezi na kuendeleza methali katika jamii ya Wanyankole.

**Maadili na Malezi katika jinsia ya Kiume**

Katika jamii ya Wanyankole, kila jinsia ilikuwa na namna ilivyoendeleza maisha yake kuhusu maadili na malezi ndani ya jamii hii. Katika kundi hili tumeweza kuona namna wanaume walivyotumia methali hizi katika majukumu yao ya kila siku.

Kinyankole: *Abashaija tibabagaya*

Kiswahili: Wanaumme hawastahili kudharauliwa.

*Kinyankole: Ibega tiringana nomutwe*

Kiswahili: Bega halilingana na kichwa.

Kinyankole: *Nyineeka kuagamba Omukazi tamugarukamu*

*Kiswahili:* Mwenye boma akiongea mwanamke hamjibu.

Kinyankole: *Taaha owasho tebarwango*

Kiswahili: Nenda kwa baba yako si chuki

Methali ya kwanza ambayo ni, *Abashaija tibabagaya* kumaanisha wanaume hawastahili kudharauliwa, ilionyesha kwamba wanaume katika jamii ya Wanyankole hawakufaa kudharauliwa na wanawake, kwa sababu ilikuwa ni kazi ya wanaume kuwalinda na kuwajibikia. Kwa hivyo mwanamke alikuwa anafunzwa kutoka utotoni ni kwa sababu gani alistahili kumheshimu mumewe. Pia mwanamke kumheshimu mumewe ilikuwa ni ishara kwamba alikuwa na maadili mazuri na hata malezi yake hayakuweza kushukiwa. Tofauti na jinsia ya kiume ambayo ilikuwa huru kuwa na maadili mazuri au la, kwa sababu malezi yao yalikuwa kwa msingi wa ubabe-dume.

Tunapotazama methali ya pili, *Ibega tiringana nomutwe* kumaanisha bega halilingani na kichwa. Tunatambua kwamba methali hii ilionyesha nafasi ya kila kijinsia katika jamii, kwani mwanaume alikuwa kichwa na mwanamke bega kwa hiyo daima mwanamke alikuwa anastahili kuwa chini ya mwanaume na mfuasi wake. Katika utamaduni wa Wanyankole, mwanaume alikuwa kiongozi na mwenye kumiliki kila kitu ndani ya boma lake mkewe akiwemo. Hii ilikuwa njia mojawapo ya kuleta amani katika jamii kwa sababu kila mtu alijua nafasi yake na majukumu yake. Tunapochungaza methali ya tatu mwanaume amesawiriwa kuwa kiongozi na aliyestahili kuheshimiwa tofauti na jinsia ya kike kwa mfano katika methali hii; *Nyineeka kuagamba Omukazi tamugarukamu* kumaanisha mwenye boma akiongea mwanamke hajibu**.** Methali hii iliweka bayana kwamba mwanamke katika jamii hii hakuwa na usemi wowote, kwa sababu hakustahili kumjibu mumewe kuhusu jambo lolote. Jamii hii iliamini kwamba, mwanamke alikuwa hana haja ya kujua kitu chochote nje ya mazingira yake ya nyumbani. Vilevile kitamaduni mwanamke mwenye maadili mazuri alikuwa mnyamavu, na mwenye kujali shughuli zake la msingi likiwa ni kumheshimu mumewe.

*Taaha omwasho tebarwango* kumaanisha nenda kwa baba yako si chuki**.** Methali hii iliweka bayana kwamba, jamii ya Wanyankole ilikuwa imejengeka kwa msingi wa mfumo wa kuumeni, pale ambapo mwanaume alikuwa amepewa uongozi na mamlaka ya jamii yote. Vilevile jamii hii iliwaruhusu wanaume kuwaoa wanawake wengi ili kuweza kupata warithi wa mali zao. Kutokana na kuzaa watoto wengi, ilikuwa ni jukumu la baba kimalezi kuwakusanya watoto wake wote na kuwaleta nyumbani ili waweze kujua nyumbani kwao. Mwanamke hakua na ukoo, ni mwanaume ambaye alikuwa na fursa hii ya kuleta watoto nyumbani. Hata hivyo, kimaadili na kimalezi ilikuwa ni jambo zuri watoto kufunzwa mambo kutokana na ukoo wao kuliko wa mama. Kwa hivyo baba kama mzazi ilibidi kuwajibikia maadili na malezi ya watoto wake tofauti na namna mama alivyokuwa anaajibikia kipengele hiki.

**Ndoa na Kazi**

Huu ni muktadha wa pili ambao ulishughulikia methali za kijinsia zinazowahusu wanaume katika jamii ya Wanyankole. Katika jamii ya Wanyankole, wanaume walikuwa wamepewa sifa za hadhi ya juu kuwaliko wanawake kama vile za uongozi na ushujaa. Kwa mujibu wa Coates (1993) tofauti za jinsia yaani ubwana wa mwanaume na unyonge wa mwanamke zinaanza siku zao za utotoni. Anasema kuwa wakiwa nyumbani, watoto hawa huwa wanafunzwa majukumu na kuumbatwa hadhi tofauti. Wasichana hubaki na mama zao huku wakifunzwa msamiati unaohusiana na upole, unadhifu na upishi. Kwa upande mwingine wavulana huandamana na baba zao na kufunzwa msamiati unaohusiana na ushujaa, ujenzi, uwindaji, ulinzi, maendeleo na uongozi. Kutokana na mawazo haya, wanaume walijipata katika hali ngumu ya kulazimika kufanya kazi kwa bidii ili kuweza kubakisha heshima katika jamii kama inavyoeleza vifuatavyo;

**Ndoa na Kazi katika jinsia ya Kiume**

Wanaume katika jamii ya Wanyankole walistahili kufanya kazi kwa nguvu na bidii kuliko wanawake. Hali hii ilichochewa na matarajio makubwa katika jamii dhidi ya jinsia ya kiume. Hili limedhihirishwa katika methali nyingi zilizojitokeza katika muktadha huu kuwahusu wanaume.

Kinyankole*: Emirimo mingi ekazibira Bigyemano okutobora omukazi*

Kiswahili: Kazi nyingi zilimzuia Bigyemano kutoboa ubikra wa mwanamke.

Kinyankole: *Omwana oine Ishe akira enaku ezakumwitsire*

Kiswahili: Mtoto aliye na baba yake huepuka majonzi ambayo yangemuua.

Kinyankole: *Omwana bamutinira obushaija bweishe*

Kiswahili: Mtoto huogopwa kutokana na uume wa babake.

Kinyankole: *Meeme mememe tezaza mwojo*

Kiswahili: Kumbembeleza hakuishi kumzaa mtoto wa kiume.

Kinyankole*: Eka effire nyineeka ayetondera abaana* kumaanisha

Kiswahili: Boma ambalo limekufa mwenye boma huomba watoto wake msamaha.

*Kinyankole: Eka eyenda kuhwaho nyineeka aimuka narya obuhoro*

Kiswahili: Boma ambalo linaelekea kufa mwenye boma huamka na kuanza kula uporo.

*Kinyankolei: Omwana oine ishe tayekorara enku*

*Kiswahili:* Mtoto ambaye ako na baba yake hawezi kubeba kuni.

Kutokana na methali hii ya kwanza *Emirimo mingi ekazibira Bigyemano okutobora omukazi* kumaanisha Kazi nyingi zilimzuia Bigyemano kutoboa ubikra wa mwanamke. Tunabaini kuwa katika jamii ya Wanyankole, kila jinsia ilikuwa imepewa kazi zake pasipo kugawana kazi hizi. Katika ugavi wa kazi hizo, mwanaume alikuwa anapewa kazi ngumu kuliko mwanamke kwa madai kwamba mwanamke alikuwa dhaifu kimaumbile. Hata hivyo, mwanaume vilevile alikuwa na jukumu kuu la kuendeleza kizazi. Kwa hivyo methali hii ilikuwa inamkumbusha mwanaume kwamba ingawa alikuwa anakazana kufanya kazi zingine, ilikuwa vizuri pia kutenga muda wa kuendeleza kizazi.

Vilevile katika methali hii, *Omwana oine Ishe akira enaku ezakumwitsire* kumaanisha mtoto aliye na baba yake huepuka majonzi ambayo yangemuua. Methali hii inaonyesha umuhimu wa mwanaume katika ujenzi wa familia inayoishi kwa furaha. Ilisadikika kuwa, maisha ya mtoto ya usoni yalitegemea rasilimali alizokuwa nazo baba yake. Kwa hivyo bado mwanaume alikuwa anakumbukushwa jukumu lake. Methali nyingine inayokaribiana kimaana na hiyo na kama vile *Omwana bamutinira obushaija bweishe* kumaanisha Mtoto huogopwa kutokana na ume wa babake. Methali hii vilevile inadai, kuwa sababu mtoto kuogopwa katika jamii hutegemea utajiri wa baba yake. Dhana 'Uume' katika muktadha huu ulimaanisha sifa na utajiri wa mwanaume. Ibainike kuwa wanawake katika jamii hii hawakuruhusiwa kuwa na mali yoyote, kwa sababu wao pia walikuwa wanamilikiwa kama kitu chochote ndani ya familia. Kwa hivyo jamii ilimtegemea mwanaume kuwe

mwenye mali nyingi na wa kusifika kumliko mwanamke. Methali nyingine zinazowasiri wanaume kuwa watu muhimu katika jamii ya Wanyankole ni kama vile:

Kinyankole: *Meeme mememe tezaza mwojo*

Kiswahili*:* Kumbembeleza hakuishi kumzaa mtoto wa kiume

Kinyankole*: Eka effire nyineeka ayetondera abaana*

Kiswahili*:* Boma ambalo limekufa mwenye boma huomba watoto msamaha

Kinyankole: *Eka eyenda kuhwaho nyineeka aimuka narya obuhoro*

Kiswahili: Boma ambalo linataka kuharibika mwenye boma huamka na kula uporo

Kinyankole*: Omwana oine ishe tayekorara enku*

Kiswahili: Mtoto ambaye ako na baba yake habebi kuni.

*Meeme mememe tezaza mwojo* kumaanisha kumbembeleza hakuishi kumzaa mtoto wa kiume. Katika kusisitiza hoja hii, waliamua kutumia mfano wa mtoto wa kiume kuonyesha umuhimu wa wanaume kufanya kazi. Kwa hivyo wanaume walikuwa wanakumbushwa kwamba ni lazima waajibike kuliko wanawake kikazi.

*Eka effire nyineeka ayetondera abaana* kumaanisha boma ambalo limekufa mwenye boma huomba watoto wake msamaha. Katika jamii ya Wanyankole neno 'kufa' ilikuwa inaashiria kwamba nyumba hiyo ilikuwa haina uongozi wowote. Ilikuwa ni jambo la aibu sana mwanaume kushindwa majukumu yake na kuanza kuwaomba watoto wake msamaha. Ishara hii ilionyesha kwamba boma hili lilikuwa halina uongozi wowote tena. Ili kuepukana na hali kama hii, wahenga wa Kinyankole waliutunga methali mbadala kuwaonya wanaume wajipange vizuri kimaisha na kuwajibikia familia zao kuzuia hali kama hizi. Methali iliyotungwa ilikuwa *ni Eka eyenda kuhwaho nyineeka aimuka narya obuhoro* kumaanisha boma ambalo linaelekea kuharibika mwenye boma huamka na kuanza kula uporo. Katika methali hii inadhihirika kwamba, dalili za kuharibika kwa boma ni mwenye nyumba kuamka na kuanza uporo. Kwa hivyo mwanaume hakustahili kufikia kiwango hiki cha kula uporo. Hivyo basi hakuwa na budi kujipanga vizuri kikazi. Hata hivyo ilikuwa ni jambo la aibu sana, mwanamke kumpa mumewe uporo katika jamii ya Wanyankole. Jambo hili lilichukuliwa kama njia moja ya kumdharau mwanaume.

*Omwana oine ishe tayekorara enku* kumaanisha mtoto ambaye ana baba yake hawezi kubeba kuni. Katika jamii ya Wanyankole ilikuwa ni jambo la aibu kubwa watoto kuanza kufanya kazi za rejareja ndani ya jamii, kama vile kubebea watu kuni, kuwachotea maji, na kulima mashamba ya wanajamii wengine iwapo baba yao angali hai. Hali hii iliashiria kwamba baba alikuwa ameshindwa kutekeleza majukumu yake. Kwa hivyo hii methali iliwachochea wanaume wafanye kazi kwa bidii ili familia na watoto wao waepukane na kazi kama hizi.

**Ndoa na Uongozi**

Jamii ya Wanyankole ilikuwa imejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni. Kumaanisha kwamba kazi zote zikiwemo za uongozi zilikuwa za jinsia ya kiume tofauti na ile ya kike. Hata hivyo, katika muktadha wa ndoa ni mwanaume ambaye alikuwa anahusika na masuala nyeti ya jamii tofauti na mwanamke aliyekuwa anahusika na mambo ya watoto nyumbani. Kwa mfano Tumusiime (1982) anasema kuwa, Mwanamme alikuwa anastahili kuongoza familia yake na vyote vilivyomo mwanamke akiwa mojawapo wa vitu vilivyomilikiwa. Kutokana na madai haya, tunatambua sababu zilizopelekea methali hizi za uongozi kutungwa kwa mkabala wa ubabe-dume katika jamii hii.

**Ndoa na Uongozi katika jinsia ya Kiume**

Mada hii imeshughulikia methali za kijinsia zilizohusu wanaume na uongozi katika jamii ya Wanyankole. Methali hizi ni kama vile:

Kinyankole: *Omushaija tahinduka omubigambo ahinduka aha kitandi honka*

Kiswahili: Mwanaumme hageuki kwenye usemi ila hugeuka kitandani tu.

Kinyankole: *Ahu abashaija batari abakazi bachwa emanja*

Kinyankole: Penye wanaumme hawapo wanawake hutoa hukumu.

*Omushaija tahinduka omubigambo ahinduka aha kitandi honka.* Methali hii inamaanisha kuwa mwanaumme hageuki kwenye usemi ila hugeuka kitandani tu. Katika methali hii imetambulika kwamba, mwanaume kama kiongozi hakustahili kugeuka kwenye usemi wake ila kwenye kitanda tu. Katika muktadha wa ndoa mwanaume alikuwa anachukuliwa kuwa kiongozi mwenye busara na hekima kuliko mwanamke katika kutoa hukumu au kauli. Kutokana na sifa ambazo jamii ilikuwa imempa, mwanamme alilazimika kufanya lolote liwalo kuhifadhi heshima zake. Hii ilikuwa na maana kuwa alipaswa kuwaza na kuwazua kabla ya kutoa maamuzi yake ambayo hayakuwa na budi kuwa mazuri Hakupaswa kughairi baada ya kufanya maamuzi. Kwani iliaminika kuwa kiongozi mzuri ni yule ambaye ana msimamo dhabiti katika uongozi wake.

*Ahu abashaija batari abakazi bachwa emanja* kumaanisha Penye wanaumme hawapo wanawake hutoa hukumu. Katika jamii ya Wanyankole ilikuwa ni jambo la aibu wanawake kutoa hukumu wanaume wakiwa wameketi. Vilevile kitamaduni ilikuwa ni mwiko mwanamke kufanya kazi hii, kwa sababu ilikuwa ni ishara kwamba mwanamme alikuwa ameshindwa. Kwa hivyo wanaume walikuwa wanatahadharishwa kutozembea katika majukumu yao, kwani wanawake wangeweza kufanya kazi zao.

**Ndoa na Utamaduni**

Jamii ya Wanyankole ni mojawapo ya jamii nyingi ulimwenguni ambayo imeweza kuhifadhi mila, desturi na imani zake kupitia utamaduni wa jamii yake. Ni jamii ambayo imetumia fasihi simulizi katika kuelemisha, kuburudishe na kuonya wanajamii wake. Vilevile kutambulika pia kama jamii iliyoendeleza kazi zake kwenye mfumo wa kuumeni. Zifuatazo ni baadhi ya methali ambazo zinadhiri usawiri wa wanaume katika ndoa na utamaduni.

**Ndoa na Utamaduni katika jinsia ya Kiume**

Katika muktadha huu tutajadili methali mbili ambazo zinahusu wanaume katika jamii ya Wanyankole. Methali hizi ni kama vile:

Kinyankole: *Empisi ekagira eti, kumbugana omushaija ashendekyerize ondijo nteraa mpunga, nkimbugana omukazi ashendekyerize ondiijo nsheeka nkaba*

Kiswahili: *Fisi alisema kwamba akimkuta mwanaumme akimsindikiza mwanaumme hujificha lakini akimkuta mwanamke akimsindikiza mwanamke mwenzake hucheka na kuvunjika mbavu.*

Kinyankole: *Oruganda rurachwekye ruzara abaishiki*

Kiswahili: *Ukoo ambao utakoma huwazaa wasichana*

Methali ya kwanza inasema, Empisi *ekagira eti, kumbugana omushaija ashendekyerize ondijo nteraa mpunga, nkimbugana omukazi ashendekyerize ondiijo nsheeka nkaba***.** Methali hii inamaanisha kuwa Fisi alisema kwamba akimkuta mwanaumme akimsindikiza mwanaumme mwenzake hujificha lakini akimkuta mwanamke akimsindikiza mwanamke mwenzake hucheka na kuvunjika mbavu. Methali hii inadhihirisha kwamba, utamaduni ulikuwa umempa mwanaume uwezo wa kuajibikia usalama wake na hata wa nyumba yake, mkewe akiwemo. Kwa hivyo mwanamke alitazamiwa kuwa jinsia ambayo ilikuwa haina uwezo wa kujilinda kutokana na hatari yoyote ndani ya jamii. Kwa hivyo hivyo, hakustahili kutoka nyumbani bila kumwambia mumewe ili ampe ulinzi. Hali hii ilionyesha kuwa mwanamke alikuwa dhaifu na alihitaji mwanaume kila wakati kuweza kumlindi.

*Oruganda rurachwekye ruzara abaishiki* methali hii inamaanisha kuwa ukoo unaelekea kuharibika ni ule ambao huwazaa watoto wasichana. Kutokana na methali hii, kitamaduni jamii ya Wanyankole ilikuwa imejengeka kwa mfumo wa kuumeni, na iliwaenzi watoto wa kiume kuliko wa kike. Kwa hivyo utamaduni ulikuwa unawaonya wanaume kuepuka kuwazaa watoto wa kike pekee. Hii ilitokana na Imani kuwa kuwazaa watoto wa kike pekee, ilikuwa ni ishara kwamba ukoo wa mwanaume ulikuwa umekomeshwa. Ili kuepuka hali hii, jamii iliwaruhusu wanaume kuwaoa wanawake wengi ili kuweza kuwapata watoto wa kiume pia. Isitoshe msichana alitazamiwa kutajirisha familia yake kwa mahari iliyotolewa ilihali kijana alikuwa anaenda kuendeleza ukoo wa baba yake.

**Ndoa na Elimu**

Jamii ya Wanyankole ilikuwa pia na njia mwafaka za kuwafundisha wanajamii wao kuhusu maisha ya kila siku na yale yajayo. Lakini mafunzo yao yalikuwa ya kijinsia, kumaanisha jinsia ya kike ilifunzwa na mama namna ya kupika, kuzaa, kulea na kumfurahisha mwanaume kingono ilihali jinsia ya kiume ilifunzwa kuhusu mambo nyeti ya jamii kama vile uongozi, uwindaji, ujenzi, uhakimu na uchinjaji. Ujinsia katika elimu ulisababisha sifa tofauti kujitokeza ndani ya jamii ya Wanyankole. Kwa mfano kutokana na madai haya, Bernard (1972) katika psychological Bulletin Vol. 35 No.3 1979} anadokeza kwamba wanaume hupendelea kutumia lugha elekezi na kwamba wao ndio hupenda kusema mambo kuhusu ukweli wa mambo (facts). Ilihali wanawake huchukuliwa kama wasiojimudu. Mtindo elekezi wa wanaume hudhihirika kupitia kwa mapenzi yao ya kufanya mihadhara, kubishana na kufanya majadiliano. Fursa ambayo wanawake hawakuweza kupewa kutokana na utamaduni ambao ulikuwa umewakweza. Kwa hivyo elimu waliyoipata ilikuwa tofauti na ilisababisha ujinsia hata katika majukumu tofauti ndani ya jamii.

**Ndoa na Elimu katika jinsia ya Kiume**

Katika muktdha huu, ni methali moja ambayo imejadaliwa katika makala hii kuonyesha jinsi wanaume walivyosawiriwa katika elimu. Katika jamii hii ni watoto wa kiume walienziwa na kupewa elimu kuwaliko wa kike. Kwa msingi kwamba watoto wa kike walikuwa ni hasara kwa wazazi. Methali hii ni kama vile "*Omwana wobwengye nahungura ebyaishe* inayomaanisha mtoto mwerevu hurithi mali ya baba yake. Katika jamii ya Wanyankole mtoto mwerevu alikuwa ni wa baba na mjinga wa mama. Kwa hivyo mtoto wa kiume ndiye aghalabu alichukuliwa kuwa mwenye akili kuliko mtoto wa kike. Kutokana na mafunzo ambayo walikuwa wanapewa, ilikuwa ni wazi mtoto wa kiume ndiye alipendelewa zaidi ya yule wa kike. Isitoshe kuhusu suala la kurithi mali, ni lazima mtoto wa kiume ndiye aliyerithishwa mali. Elimu aliyopewa mwanamke ilikuwa inahusu mambo yasiyokuwa na hadhi ya juu katika jamii kama vile upishi na kadhalika. Jamii ya Wanyankole ilikuwa haithamini jinsia ya kike kupata elimu mahususi kwa madai kwamba, mtoto wa kike angeolewa na kufaidisha upande wa mumewe. Isitoshe mtoto wa kike pia alitazamiwa kuwa njia moja ya kuleta utajiri nyumbani, kwa sababu alipoolewa alileta mahari nyumbani. Kwa hivyo ilikuwa ni kazi bure kumwelemisha mtoto wa kike katika jamii ya Wanyankole. Kwa msngi huu, elimu waliyoipata ilikuwa tofauti na ilisababisha ujinsia hata katika majukumu tofauti ndani ya jamii.

**Ndoa na Uchumi**

Jamii ya Wanyankole kama mojawapo ya jamii nyingi za Kiafrika ilikuwa inajivunia kipato kutokana na ufugaji wa ng'ombe wao. Ng'ombe hawa walikuwa ni njia mojawapo ya kuendeleza uchumi wao kama jamii. Waliweza kuwauza, kutoa mahari, kupata maziwa na kuuza nyama yenyewe. Isitoshe kando na uuzaji wa ng'ombe hao, pia jamii hii ilikuwa inalima vyakula vidogo vidogo kama vile mtama, wimbi, maharagwe na viazi vitamu na kuweza kuongezea kwa uchumi wao. Ni vizuri ieleweke kwamba, uchumi huu pia ulikuwa ni wa kijinsia pale ambapo wanaume walikuwa wafugaji nao wanawake wakulima.

**Ndoa na Uchumi katika jinsia ya Kiume**

Katika muktadha huu methali mbili za kijinsia zilizowahusu wanaume zilijadiliwa katika jamii hii. Ilitambulika kuwa wanaume walikuwa wakijihusisha na uchumi wa kifahari kuwaliko wanawake. Hii ni kumaanisha kuwa wanaume walikuwa wafugaji wa ng'ombe ilhali wanawake walikuwa wakulima wa vyakula vya kipato kidogo ndani ya jamii. Methali hizi ni kama vile:

Kinyankole: *Kiburwa ente kiburwa Omukazi*

Kiswahili: Akosaye ng'ombe hukosa mke.

Kinyankole: *Okukunda akuha ente otayenda kuofa akuha Omukazi*

Kiswahili: Akupendaye hukupa ng'ombe asiyetaka ufe hukupa mke.

Methali ya kwanza ni, *Kiburwa ente kiburwa Omukazi* yaani Akosaye ng'ombe hukosa mke. Kutokana na uchumi wa jamii hii ambao ulikuwa ufugaji wa ng'ombe, ilikuwa ni kosa kubwa mwanaume kukosa ng'ombe. Kwa sababu kutokana na ukosaji wa ng'ombe hakuweza kupata pesa za

mahitaji ya nyumbani na vilevile mahari ya kutoa ndiposa apewe mke. Kwa hivyo ilimbidi mwanaume kufanya kazi kwa bidii ili kuweza kujiendeleza kiuchumi ndani ya jamii. Jambo ambalo lilikuwa tofauti na mwanamke kwa sababu, katika jamii hii mwanamke hakuruhusiwa kujihusisha na masuala ya biashara. Kwa hivyo mwanamke alikuwa hana uwezo wa kujiendeleza kiuchumi kama mwanaume.

Methali nyingine inayomsawiri mwaname katika mkabala wa uchumi ni *Okukunda akuha ente otayenda kuofa akuha Omukazi* inayomaanisha Akupendaye hukupa ng'ombe asiyetaka ufe hukupa mke. Katika jamii hii, ng'ombe walitumiwa kama njia moja ya kupata kipato cha jamii, na vilevile pia waliwatumia kuleta undugu. Kando na uchumi, ng'ombe hawa walitumiwa kulipa mahari ya watoto wao, na hata rafiki zao ambao walikuwa wanataka kuoa. Isitoshe kuna uchumi wa aina nyingine ambao jamii hii ilikuwa inautumia, tofauti na ule wa kupewa pesa moja kwa moja. Kwa mfano ikiwa rafiki yako amekupa ng'ombe leo, baada ya kipindi fulani wewe pia ulilazimika kumpa pia ng'ombe kama zawadi. Kwa hivyo wanajamii ambao walikuwa hawana pesa walitumia mbinu hii na mwishowe waliweza kuwa na ng'ombe wengi ambao waliwauza na kuweza kuendeleza uchumi wao.

**Hitimisho**

Kwa kuhitimisha makala imeweka bayana namna methali za kijinsia zimejitokeza katika miktadha tofauti ndani ya jamii hii. Ilibainika kuwa miktadha hii ilichangia katika methali hizi kuweza kuonyesha namna mwanaume alivyosawiria katika jamii. Sawia na jamii zingine za kiafrika, Wanyankole waliwaenzi wanaume na kuwapa hadhi ya juu ikilinganishwa na wanawake waliyopewa. Methali zilizohakikiwa na kujadiliwa katika Makala hii zinadhihiri kuwa wanaume walitamalaki katika asasi za kijamii kama: Ndoa, utamaduni, uongozi, elimu na uchumi. Vilevile wanaume walihusika katika malezi na maadili japo katika kiwango cha tathmini. Ni wanawake ndiyo waliopaswa kuwalea watoto na kuwafundisha maadili. Hata hivyo watoto waliolelewa vizuri na kupata maadili walinasibishwa na baba yao ilihali wale waliyotuvuka kimaadili walihusishwa na mama yao. Hali inaonyesha kukithiri kwa taswira dumifu za kijinsia katika jamii ya Wanyankole inayodhirika kupitia methali za kujinsia. Hata hivyo, utafiti huu unakubaliana na imani kwamba jamii ya Wanyankole kama ilivyo jamii yoyote ile imebadilika na hivyo kutokana na ukale wa methali hizi za kijinsia, yamkini jamii ya sasa ina taswira na mitazamo mipya kuhusu usawiri wa mwanamme na mwanamke. Kwa hivyo utafiti huu unapendekeza kuwepo kwa tafiti endelezi kubaini iwapo mabadiliko ya kisasa na utandawazi umeathiri usawiri wa wanaume na wanawake katika methali za kisasa za Wanyankole.

**Marejeleo**

Bernard, J. (1972). The Sex Game. New York: Atheneum.

Chafetz, J. (1974). *Masculine / Feminine or Human?* Itasca, IL: Peacock Publishers. Fetter lane.

Coates, J. (1986). Women, Men and Languages:A sociolinqustic account of sex difference language. London: Longman Group

Finnegan, R. (1992). *Oral Tradition &verbal Arts*. London: Routledge press, New Gokumanya Publishers.

Izugbara, C. O. (2005). "Hypothesis on the Origin of Hegemonic Masculinity" *In Sexuality in African Magazine*. Lagos Africa Regional Sexuality Resource Centre 2(1), 13-14.

Kibigo, M. L. (2019). *Ubabedume katika Majigambo ya Miviga ya Shilembe na Mchezasili wa Mayo ya Waisukha Nchini Kenya kwa Mtazamo wa Kisemantiki. (*Tasnifu ya Uzamifu ambayo imewasilishwa kwa East African Journal of Swahili Studies, 4(1), 2019

Lubuuka. Y: "*Usawiri wa mwanamke katika Methali za Wanyankole*." Uganda:

Lukamika, M. K, Choge, S. C., & Simiyu , F. W. (2019). Tamathali za Semi Zinazosawiri

Ubabedume katika Majjigambo ya Miviga ya Shilembe na Mchezasili wa *Mayo* ya Waisukha, Nchini Kenya kwa Mtazamo wa Semantiki. Tasnifu ya Uzamifu iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia.

Maingi, R., (2005). "The Kenyan Constitutional Reforms Process" A Case Study on the Work of PIDA Kenya in Securing Womens Right' *Feminist Africa*

Ruether, R. (1974). *Religion and Sexism.* New York: Simon and Schuster.

Seita A. (1987). *Efumu Omurunyankole Rukiga, Omuhanda*. Mbarara:

Sokoloff, N. (1980). *Between Money and Love*. New York: Praeger.

Wandera, S. P. (1996). *Usawiri wa Mwanamke Katika Ushairi wa Kiswahili 1800-1900: Uhalisia au Ugandamizaji? Tasnifu ya M.A, Chuo kikuu cha Egerton.*

Wells-Wilbon, R na Holland, S. (2001). *Social learning theory and the Influence of male role models on African American children in PROJECT 2000.*